## Njia ya Wokovu

Njia ya Kuingia Katika ufalme wa Mungu ni Kwa imani. Imani hii inahusikana kwa kuamini katika neno lake- 'Biblia' - na kuitii vile inavyosema yakuwa wanaume na wanawake watubu dhambi zao na kubatizwa na kumfuata Yesu kwa uaminifu.

*(Waebrania 11:16; 1 Wathesalonike 2:13; 2 Timotheo 3:15; Matendo 2:37; Marko 16:16; Yohana 13:3-5; Mathayo 16:24-27)*

## WaKristadelfiano Wanakaa Maisha ya aina gani ?

Njia ya Mungu ya wokovu inatupa uwelekezo Maalumu katika Maisha yetu. Tunajaribu kujiweka kwa Mungu na msimamo ambao una nguvu, katika maombi na kazi njema pamoja na hayo tunajua yakuwa wokovu ni kwa neema.

*(Wakolosai 1:3-11; 1 Petro 2:1-5; 2 Petro 1:5-11; Yakobo 2:17, 5:16; Waefeso 2:5-10)*

Katika uwezo wa Mungu tunajaribu kumpendeza siku zote, tunajaribu kuwa kama Kristo ambaye alimtii Babaye na bila kujipenda akajjpeana kwa wanadamu.

*(Wafilipi 2:13; 4:13; Waefeso 3:20; 2:1-5; Warumi 12:1-2; Waefeso 5:1-2)*

Tunajipeana kwa nguvu Katika kazi na uwaaminifu katika ndoa na kupeana kwa ukarimu na katika kuhubiri, na kuwa wachangamufu katika maisha na furaha katika Mungu wetu.

*(Waefeso 5:5; 2 Timotheo 4:1-5; Yohana 16:33; Mathayo 5:1-16; Wafilipi 4:4-7)*

Wakristadelfiani wanaweza kupatikana kwa sanduku la posta lifatao.

# MASWALI YAKO YAJIBIWA KUHUSU KANISA LA KIKRISTADELFIANO

## **Wakristadelfiani ni akina nani? Je. ni Wapya?**

Wakristadelfiani ni Kundi ndogo la Wakristo ambao wamechukua imani na mfano wa Kanisa la kwanza aliyeliwacha Kristo. Kundi hili la Wakristadelfiano limekuwepo zaida ya miaka mia moja. Maana ya jina Kristadelfiano ni 'Ndugu katika Kristo'.

*(Waebrania 2: 11; Marko 3:34-35; Mathayo 25:40)*

## Wakristadelfiano wapatikanakje?

Tuko pahala popote ulimwenguni. Kama vile Wakristo wa kwanza walivyokuwa, tunakutanika katika nyumba zetu, na wakati mwingine katika machumba yakukodisha, au zebuleni zetu za mikutano.

*(Matendo 1:13, 2:46, 18:7, 19:9, 28:30)*

## Wakristadelfiano wanajiunuga je?

Sisi huwa kama ya jamii mtu mmoja na kila mtu kwa kila kundi anaitwa Ndugu au Dada na wote wana mamlaka moja kuhusu maendeleo ya mikutano. Imani moja yenye nguvu inatuunganisha pamoja katika Undugu.

*(Mathayo 23:8-12: Warumi 12:4-6, 16:1; I Wakorintho 12:4-27; Wagalatia 3:28)*

## Wakristadelfiano Huamini nini na Kufunza

Tunaamini ya kuwa Biblia ndio habari pekee ambayo Mungu amedhihirisha kwa wanadamu, ili kumleta kila mtu kuitii kwa imani. Biblia ndio uwezo na tunafunza isomwe kwa kusali na kwa uangalifu katika nafasi ipatikanapo.

*(Warumi 16:26; Yohana 17:17; Matendo 17:11)*

Mafunzo ya muhimu ni kama yafuatayo.

## Mwenyezi Mungu

Kuna Mungu mmoja wa pekee asiyeweza kuona uharibifu na **Yesu Kristo** ni mwana wake wa pekee, na Roho mtakatifu ni nguvu zake.

*(Isaya 45:5; 1 Timotheo 1:17; Waefeso 4:6; Luka 1:35; Matendo 1:8; Luka 24:49)*

## Mwanadamu

Mwanadamu anakufa na ni mwenye dhambi mbele ya mwenyezi Mungu. Utu wake wote ni wa dhambi, na dhawabu yake ni mauti, kufa kabisa mwisho wa maisha yake.

(Ayub 4:17; Warumi 3:23, 6:23; Yeremia 19:9; Marko 4:17; Mhubiri 9:1-6; Zaburi 146:3-4)

## Yesu

Kwa mapenzi yake Mungu alimtuma Mwanadamu Yesu katika ulimwengu kuwaokoa wanadamu kutoka kwa dhambi zao. Waaminio katika yeye wasife bali wapate uzima wa milele.

*(Mathayo 1:21; Yohana 3:16)*

## Tumaini

Tumaini ya pekee ya uhai baada ya kifo ni Ufufuo wa Mwili na uzima wa milele katika ufalme wa Mungu Duniani.

*(Zaburi 49:12-20; 1 Wakorintho 15:12-50; Warumi 8:23-35; Matendo 24:15; Yohana 11:25; Ufunuo 5:10, 20:4)*

## Dhabihu ya Kristo

Yesu hakuwa na dhambi. Alikufa kuonyesha haki ya Mungu na kuokoa wale wanaopokea dhabihu hii kwa njia ya imani. Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, na kumpa kutoharibika na uwezo katika mbingu na duniani, na kumweka kuwa mpatanishi mbinguni kati ya Mungu na Wanadamu.

*(Matendo 2:23-36; Waefeso 1:19-23; 1 Timotheo 2:5; Waebrania 4:14-16; Warumi 3:21-26)*

## Kurudi kwa Yesu

Yesu yuaja tena duniani. Wakati huo atawafufua wengi wa waliokufa kuwahukumu pamoja na walio hai. na kuwapa wafuasi wake halisi wenye imani uhai na uzima wa milele katika ufalme wa Mungu.

*(Ufunuo 22:12; Luka 21:20-32; Yohana 5:28-29; Danieli 12:2; 2 Timotheo 4:1; Mathayo 25:34)*

## Ufalme wa Mungu

Ufalme wa Mungu utasimamishwa hapa duniani Yesu Kristo atakuwa mfalme. Mji wake mkuu utakuwa YERUSALEMU na milki yake itakuwa ulimwengu wote, na serikali yake italeta haki na amani bila kikomo.

*(Danieli 2:44, 7:27; Matendo 3:21; Yeremia 3:17; Zaburi 72:1; Danieli 7:14; Isaya 9:6-7, 11:9, 61:1-11)*

## Ahadi

Injili haiwezi kutenganishwa na ahadi za Mungu alizomuahidi Ibrahimu na Daudi katika nyakati za agano la kale. Ahadi hizi zilitimilika katika Yesu Kristo.

*(Wagalatia 3:6-9, 25; Luka 1:31-33; 2 Peter 1:4; Mwanzo 13:14, 17:1, 22:15-18; 2 Samueli 7:12-16)*